# SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### TAASISI YA UTAFITI WA AFYA


3. Kuanzisha Taasisi.
4. Muhuri na nembo ya Taasisi.
5. Malengo ya Taasisi.
6. Kazi za Taasisi.
7. Uwezo wa Taasisi.


### SEHEMU YA TATU
### UTAWALA NA UENDESHAJI WA TAASISI


8. Uanzishaji na muundo wa Bodi.
9. Katibu wa Bodi.
10. Kazi za Bodi.
11. Uwezo wa Bodi.
12. Mikutano ya Bodi.
13. Makamu Mwenyekiti.
14. Akidi ya mkutano.
15. Maamuzi ya Bodi.

16. Muda wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi.

17. Taratibu za mikutano.

18. Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

19. Stahiki za wajumbe.

20. Mjumbe mualikwa.

21. Mgongano wa maslahi.

22. Kukasimu kazi za Bodi.

23. Kumsitisha au kumsimamisha mjumbe wa Bodi.

24. Kamati za Bodi.

**SEHEMU YA NNE**
**MKURUGENZI MKUU NA WATUMISHI WENGINE WA TAASISI**

25. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

26. Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

27. Watumishi wa Taasisi

**SEHEMU YA TANO**
**SAMPULI ZA KIBAOLOJIA KWA AJILI YA UTAFITI WA AFYA, NA UTAFITI KATIKA DAWA ZA KIASILI NA TIBA MBADALA**

28. Madhumuni ya ukusanyaji wa sampuli za kibaolojia.

29. Hifadhi ya sampuli za kibaolojia.

30. Kusafirisha na kuingiza sampuli za kibaolojia.

31. Udhibiti wa sampuli za kibaolojia.

32. Utafiti katika tiba asili na mbadala.

**SEHEMU YA SITA**
**HAKI MILIKI**

33. Haki miliki.

### SEHEMU YA SABA
### MASHARTI YA FEDHA


34. Fedha za Taasisi.

35. Makadirio ya mapato na matumizi.

36. Hesabu na ukaguzi.

37. Ripoti ya utekelezaji wa mwaka.

38. Kufungua hesabu ya benki.


### SEHEMU YA NANE
### MAKOSA NA ADHABU


39. Makosa na adhabu.

40. Adhabu ya jumla.


### SEHEMU YA TISA
### MASHARTI MENGINEYO


41. Uchunguzi wa majaribio ya dawa.

42. Kanuni.

43. Kufuta na Kubakiza.

**SHERIA NAM. 5 YA 2020**

NIMESAINI

{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

5 Mei ..................................................., 2020

# SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar, 2020 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokua kama itaelezwa vyenginevyo:

"mtaalamu wa tiba mbadala" maana yake ni mtu aliyepata mafunzo rasmi na aliyepata elimu, ujuzi na umahiri katika utendaji wa kada ya tiba mbadala kama inavyotambuliwa kitaifa na kimataifa;

"tiba mbadala" maana yake ni kiwango cha jumla cha elimu na utendaji unaotumika katika uchunguzi, kinga, tiba na kutokomeza matatizo ya kimwili, kiakili na kijamii yanayoendana kikamilifu kutokana na mifumo mbali mbali ya tiba mbadala iliyoanzishwa katika kada husika;

“mnyama" maana yake ni kiumbe chochote chenye uti wa mgongo na kisichokuwa na uti wa mgongo au wanyama wengine isipokuwa binadamu;

“mnyama husika” maana yake ni mnyama ambaye hutumika kwa ajili ya utafiti wa afya au uchunguzi wa majaribio ya dawa;

“benki ya kibaolojia” maana yake ni ukusanyaji wa sampuli za kibaolojia na taarifa zinazohusiana ambazo zinahifadhiwa katika mfumo uliyoandaliwa;

“sampuli za kibaolojia” maana yake ni viungo na sehemu za viungo, chembe chembe hai, tishu, muundo wa chembe chembe hai ndogo, mazalio ya chembe chembe hai, damu, mate, virusi, kohozi, mbegu za uzazi, kiinitete, tishu za mtoto mchanga aliye tumboni, na mabaki ikiwemo mkojo, kinyesi, jasho, nywele, magamba ya ngozi, maoteo ya kucha, fuko la uzazi na chembe chembe hai zilizojikusanya kutoka kwa binadamu au tishu za mnyama;

“zalio la damu” maana yake ni zalio lolote linalotokana au linalozalishwa kutokana na damu, ikijumuisha chembe chembe hai mama zinazozunguka, chembe chembe hai mama za uboho na chembe chembe hai mama za ukamba;

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 8(1) cha Sheria hii;

“uchunguzi wa majaribio ya dawa” maana yake ni utafiti wenye mfumo maalum, unaojumuisha ushiriki wa binadamu au wanyama husika, ambao unatoa majibu ya maswali maalum kuhusiana na usalama au ufanisi wa dawa, chanjo au njia za kujikinga au matibabu;

“Mwenyekiti” maana yake ni Mwenyekiti wa Bodi anayeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 8(1)(a) cha Sheria hii;

“Mkurugenzi Mkuu” maana yake ni Mkurungenzi Mkuu wa Taasisi anayeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 25(1) cha Sheria hii;

“sampuli za urithi” maana yake ni sehemu ya chembechembe hai ambazo zinabeba taarifa za kibaolojia zinazopitishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kwengine;

“Serikali” maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

“kituo cha afya” maana yake ni majengo ya umma au binafsi au maeneo mengine yanayoendeshwa au yaliyoandaliwa kutoa matibabu ya wagonjwa wa ndani

au nje, uchunguzi au kuchukua hatua za matibabu, uuguzi, urekebishaji, uangalizi maalum, urejeshaji hali, uzuiaji au huduma nyengine za afya;

"utafiti wa afya" maana yake ni kazi yoyote inayofanywa ambayo:

(a) inachangia maarifa ya kibaolojia, uchunguzi, saikolojia au mwenendo wa kijamii kwa wanadamu au wanyama;

(b) inatumia njia za kisayansi kupata taarifa zinazohusika na afya na maradhi;

(c) inaendeleza njia za kisayansi kwa ajili ya utoaji huduma za kiafya na uchunguzi wa binadamu;

(d) inachunguza sababu za maradhi na athari za mazingira kuhusiana na mwili wa binadamu; au

(e) inaendeleza matumizi mapya ya kifamasia, dawa na teknolojia ya afya;

"binadamu mshiriki" maana yake ni mtu yeyote anayeishi ambaye anaridhia kushiriki katika kazi ya utafiti wa afya au mwili wa mtu aliyekufa au sehemu ya mwili wa mtu aliyekufa;

"Taasisi" maana yake ni Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"haki miliki" maana yake ni haki ya kipekee inayotolewa kwa mvumbuzi na mmiliki wa kazi ambazo zinatokana na matokeo ya ubunifu ya uwezo kwa kibinadamu;

"makubaliano ya kusafirisha sampuli" maana yake ni mkataba ulioandikwa baina ya mtoaji na mpokeaji wa sampuli ya utafiti;

"dawa" maana yake ni dawa ya binadamu, dawa ya mnyama, zalio la dawa, dawa asili au kitu chochote au mchanganyiko wa vitu kwa ajili ya matumizi ya binadamu au mnyama, au inayokusudiwa kutumika au kutengenezwa kwa ajili ya matumizi ya matibabu kwa ufanisi wake au kwa madhumuni ya kifamakolojia katika uchunguzi, utabibu, uondoaji, urekebishaji au ukingaji au hali isiyo ya kawaida ya kimwili au kiakili au dalili za maradhi kwa binadamu au mnyama;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya afya;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"pendekezo la utafiti" maana yake ni pendekezo la utafiti wa kiafya lililoidhinishwa na Bodi;

"mtafiti" maana yake ni mtu ambaye anafanya utafiti wa kitaaluma na kisayansi;

"Katibu" maana yake ni Katibu wa Bodi anayeteuliwa chini ya kifungu cha 9(1) cha Sheria hii;

"tiba za asili" maana yake ni mchanganyiko wa taaluma na utendaji, ama unafahamika au vinginevyo, unaotumika katika uchunguzi, ukingaji au uondoaji maradhi ya kimwili, kiakili au kijamii na ambao unaendana sambamba na uzoefu uliopita na maoni yanayotolewa kutoka kwenye kizazi kwenda kizazi chengine, kwa maneno au maandishi;

"mtabibu wa tiba asili" maana yake ni mtu ambaye anatambulika na jamii au Baraza la Tiba Asili ambapo mtu huyo anaishi kama mtaalamu anayetoa huduma ya afya, kwa kutumia mboga mboga, vitu vinavyotokana na wanyama au madini na njia nyengine zozote zinazotokana na jamii, utamaduni na historia ya dini na utaalamu, tabia na imani ambazo zinazofuatwa katika jamii kuhusiana na ustawi wa mtu kimwili, kiakili na kijamii, zikiwemo sababu za maradhi na ulemavu.

**SEHEMU YA PILI**
**TAASISI YA UTAFITI WA AFYA**

Kuanzisha Taasisi.

**3.**-(1) Kutakuwa na Taasisi itakayojulikana kama Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar.

(2) Bodi inaweza kuamua jina fupi kwa ajili ya matumzi bora ya Taasisi.

(3) Taasisi itakuwa ni chombo kinachojitegemea kwa baadhi ya mambo, na kwa ridhaa ya Waziri, itakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(b) kuingia kwenye mkataba wowote au muamala kwa jina lake kwa mujibu wa sheria zilizopo;

(c) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(d) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo taasisi kwa asili yake kisheria inastahiki kutekeleza au kufanya.

Muhuri na nembo ya Taasisi.

**4.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Taasisi katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Taasisi katika waraka wowote yatathibitishwa na saini ya Mkurugenzi Mkuu au afisa mwingine yeyote wa Taasisi aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Taasisi utawekwa muhuri wa Taasisi na utathibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya Taasisi.

**5.** Malengo ya Taasisi yatakuwa yafuatayo:

(a) kukuza, kusaidia na kufanya utafiti ambao unakidhi viwango vya juu vya kisayansi na maadili vya kitaifa na kimataifa ambavyo vinaendana na nyanja zote za afya;

(b) kukuza matumizi ya matokeo ya utafiti kwa ajili ya ushahidi wa tukio;

(c) kutoa utaratibu wa kuhakikisha kwamba utafiti wa afya unafanyika Zanzibar:

(i) kuendana na vipaumbele vya kitaifa vya utafiti wa afya na sera za kitaifa;

(ii) kutatua matatizo ya kiutafiti wa afya yalioainishwa kitaifa na kimataifa;

(d) kuainisha, kukuza na kuendeleza vipaji maalumu miongoni mwa watafiti wa afya kwa lengo la kuendeleza watafiti wengi wa sayansi ndani ya Zanzibar; na

(e) kuhamasisha utafiti wa ushirikiano baina ya watafiti waliopo katika Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar na watafiti wa taasisi nyengine za utafiti na maendeleo ndani na nje ya Zanzibar;

Kazi za Taasisi.

**6.** Kazi za Taasisi zitakuwa zifuatazo:

(a) kutekeleza na kukuza utafiti katika nyanja zote za afya na utekelezaji wa tiba za asili kwa madhumuni ya kurahisisha maendeleo na kuchukua hatua za kukinga, kutibu na kurekebisha utendaji wa kiafya na dawa za asili;

(b) kukagua taasisi yoyote au eneo lililoruhusiwa na Taasisi kwa ajili ya kufanya utafiti wa afya, ikijumuisha kanzidata na benki za kibaolojia;

(c) kutoa nyenzo na programu za mafunzo kwa ajili ya mtaalamu wa ndani kutekeleza utafiti wa kisayansi unaohusiana na afya na sayansi shirikishi;

(d) kupitia mapendekezo yote ya tafiti za afya na kuhakikisha kwamba hazina madhara au hatari na zina maslahi kwa watu wa Zanzibar;

(e) kufuatilia, kudhibiti na kuratibu utafiti wa afya unaofanywa kwa niaba ya au kwa maslahi ya watu wa Zanzibar;

(f) kuanzisha mfumo wa kusajili matokeo, mifumo ya uendeshaji wa nyaraka na usambazaji wa taarifa kwa umma, Serikali, jumuiya za kimataifa za utafiti, taasisi za kujitolea na sekta binafsi kuhusiana na nyanja zote za utafiti wa afya zinazofanywa Zanzibar;

(g) kubeba jukumu kwa ajili ya kudhibiti kituo chengine kinachoweza kuanzishwa na Taasisi au kupewa jukumu na Taasisi;

(h) kuhakikisha uwazi na uwajibikaji kwa Wazanzibari kwa ajili ya uwekezaji katika utafiti wa afya;

(i) kuanzisha miundo na mifumo ya utawala bora kwa utekelezaji mzuri wa Taasisi;

(j) kushauri, kushirikiana na kuunda ubia pamoja na watu au taasisi za ndani au nje ya Zanzibar ambazo zina maslahi katika mambo yanayohusiana na afya au utafiti wa afya;

(k) kuwezesha midahalo baina ya watunga sera, watafiti katika kada mbali mbali, wahudumu wa afya na jamii ili kuhakikisha kwamba utafiti unaendana na mahitaji ya watu na kwamba matokeo ya utafiti yanatumika kwa wadau husika kwa ajili ya kuimarisha maisha ya watu;

(l) kusajili watafiti wa afya wanaofanya tafiti za afya;

(m) kuanzisha mfumo wa udhibiti wa ubora wa utafiti;

(n) kuainisha fursa za afya zinazojitokeza, tishio na changamoto na kuharakisha uvumbuzi wa tiba na matibabu na kuimarisha huduma ya afya, kinga na mikakati bora;

(o) kuhamasisha mijadala ya masuala ya maadili na matumizi ya misingi ya maadili kwa utafiti wa afya;

(p) kutumia fursa na kutoa msaada kwa ajili ya ushiriki wa wanasayansi wa Zanzibar katika mashirikiano ya kimataifa na ubia katika utafiti wa afya;

(q) kushirikiana na Serikali au mtu yeyote au Taasisi, katika kukuza utafiti wa afya;

(r) kufuatilia uchunguzi wa majaribio ambao unafanywa Zanzibar; na

(s) kufanya kazi nyengine zozote zinazoweza kuelekezwa na Waziri.

Uwezo wa Taasisi.

**7.**-(1) Taasisi inaweza:

(a) kumtaka au kumlazimisha mtafiti wa afya yeyote au taasisi yoyote ya utafiti kuwasilisha taarifa au kumbukumbu ambazo ni muhimu kuiwezesha taasisi kufuatilia utekelezaji au shughuli za mtafiti wa afya au taasisi ya utafiti;

(b) ikiwa maadili yamevunjwa, kuwasimamisha watafiti wa afya na taasisi za utafiti kufanya kazi za utafiti Zanzibar;

(c) kutaifisha, kuzuia na kuharibu, pale itakapobidi, sampuli za kibaolojia zilizopatikana kwa mtu yeyote aliyekwenda kinyume na sharti lolote la Sheria hii; na

(d) kumtaka mtafiti wa afya yeyote ambaye, au taasisi ya utafiti ambayo ipo katika udhibiti wa shughuli ya utafiti wa afya kutoa taarifa kwa Taasisi kuhusu dhamira ya kuhama kutoka eneo la awali kwenda eneo jengine.

(2) Taasisi inaweza kumuidhinisha afisa yeyote kufanya ukaguzi kwa muda muafaka, eneo lolote, sehemu ya kuingilia na sehemu ya kutokea.

## SEHEMU YA TATU
## UTAWALA NA UENDESHAJI WA TAASISI

Uanzishaji na muundo wa Bodi.

**8.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi itakayoundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kitaifa ya Maradhi ya Binadamu;

(d) Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya;

(e) Mwakilishi kutoka Skuli ya Tiba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA);

(f) Mwakilishi mmoja kutoka maabara ya uchunguzi; na

(g) Wajumbe wengine wawili, mmoja miongoni mwao atatoka sekta binafsi;

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi akiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya utawala wa afya, sayansi ya afya au fani nyengine yoyote inayohusiana nayo kutoka katika taasisi inayotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka kumi katika utumishi wa umma; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

(3) Ukitoa Mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, taaluma na usawa wa kijinsia.

Katibu wa Bodi.

**9.**-(1) Bodi itamteua Afisa wa Sheria ambaye ni muajiriwa wa Taasisi mwenye angalau Shahada ya Kwanza ya Sheria na uzoefu usiopungua miaka mitatu kuwa Katibu wa Bodi:

(2) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi, na atahusika na:

(a) kuchukua kumbukumbu sahihi za mikutano ya Bodi;

(b) kutunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(c) kutoa taarifa sahihi za mikutano ya Bodi kwa wajumbe;

(d) kutoa ushauri sahihi kwa Bodi pale unapohitajika; na

(e) kufanya kazi nyengine kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

**10.** Kazi za Bodi zitakuwa zifuatazo:

(a) kusimamia na kufuatilia uendeshaji na utekelezaji wa Taasisi;

(b) kumshauri Waziri kutokana na jambo lolote linalohusiana na utafiti wa afya au sera ya afya na masuala ya mikakati yanayohusiana na utafiti wa afya;

(c) kupitia na kuidhinisha sera, kazi na mipango ya uendeshaji, bajeti, ripoti na taarifa za fedha zilizokaguliwa za Taasisi;

(d) kupendekeza kwa mamlaka husika jambo lolote linalohusiana na maslahi au taratibu nyengine na masharti ya huduma za watumishi wa taasisi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

(e) kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali;

(f) kutunga na kusimamia kanuni za watumishi na kanuni za fedha za Taasisi;

(g) kupitia na kuidhinisha malengo, shabaha na hatua za utekelezaji wa Taasisi kuendana na:

(i) mpango mkakati wa Taasisi;

(ii) mpango wa mwaka wa Taasisi; na

(iii) mkataba wa utekelezaji;

(h) kutoa masharti na taratibu za motisha kwa huduma iliyotolewa na watafiti kwa ajili ya kuhamasisha kufanyika tafiti na utoaji wa zawadi kwa matokeo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma; na

(i) kutekeleza kazi nyengine zozote zilizoainishwa katika Sheria hii au ambazo zinaweza kuwa ni muhimu kwa ajili ya kufikia malengo ya kuanzishwa Taasisi.

Uwezo wa Bodi.

**11.** Bodi itakuwa na uwezo wa jumla wa kusimamia kuhusiana na utekelezaji wa kazi za Taasisi, na kwa mahsusi itakuwa na uwezo wa:

(a) kupendekeza muundo wa kitaasisi wa Taasisi kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma;

(b) kupendekeza kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuhusiana na taratibu na masharti ya utumishi ya watumishi wa Taasisi;

(c) kuajiri au kuteua wafanyakazi wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(d) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mfanyakazi yeyote kwa kosa la kuvunja maadili kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake; na

(e) kuidhinisha ada na tozo nyengine za huduma zinazotolewa na Taasisi.

Mikutano ya Bodi.

**12.**-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote pale inapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

(2) Mikutano yote ya Bodi itaitishwa na kuendeshwa na Mwenyekiti.

(3) Endapo Mwenyekiti atakuwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataitisha na kuendesha mkutano wa Bodi.

(4) Endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliopo watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha mkutano, na mjumbe aliyechaguliwa atatekeleza mamlaka na majukumu yote ya Mwenyekiti.

Makamu Mwenyekiti.

**13.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Akidi ya mkutano.

**14.** Zaidi ya nusu ya wajumbe wataunda akidi ya mkutano wowote wa Bodi.

Maamuzi ya Bodi.

**15.** Bodi itafanya maamuzi yake kwa makubaliano, na ikitokezea kutokubaliana, uamuzi utafikiwa kwa kura, na ikitokezea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

16.-(1) Mwenyekiti wa Bodi atashika nafasi kwa kipindi cha miaka minne kutoka tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Muda wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi.

(2) Isipokuwa kwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Taratibu za mikutano.

17. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kutengeneza taratibu zake kuhusiana na mikutano na utekelezaji mzuri wa kazi zake ikijumuisha kamati za Bodi.

Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

18. Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi ikiwa mjumbe huyo:

(a) amefariki;

(b) ameshindwa kuhudhuria mikutano mitatu ya Bodi mfululizo bila ya sababu ya msingi;

(c) amejiuzulu au kwa namna yoyote amepoteza sifa ya ujumbe wa Bodi; au

(d) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili.

Stahiki za wajumbe.

19. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa stahiki zao kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Mjumbe mualikwa.

20. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Bodi kuhudhuria majadiliano yoyote ya mkutano wa Bodi kama mtaalam, lakini mtu huyo aliyealikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Mgongano wa maslahi.

21. Mjumbe ambaye ana maslahi moja kwa moja au vyenginevyo katika mkataba au mkataba unaopendekezwa au jambo lolote linalojadiliwa na Bodi, atatangaza asili ya maslahi yake kwa Bodi na Bodi itamuondoa katika ushiriki wa majadiliano ya jambo hilo.

Kukasimu kazi za Bodi.

22. Bodi inaweza, ikiwa itaona inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Mkurugenzi Mkuu, kamati au mtumishi mwingine yeyote wa Taasisi.

Kumsitisha au kumsimamisha mjumbe wa Bodi.

**23.** Waziri anaweza kumsitisha au kumsimamisha mjumbe yeyote wa Bodi isipokuwa Mwenyekiti na mjumbe anayeingia kwa nafasi yake ikiwa mjumbe huyo:

(a) hawezi kutekeleza kazi za nafasi yake;

(b) ametiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusisha udanganyifu, kutokuwa muaminifu au uvunjifu wa maadili; au

(c) ameshindwa kuhudhiria mikutano mitatu ya Bodi mfululizo bila ya idhini ya Mwenyekiti.

Kamati za Bodi.

**24.**-(1) Bodi inaweza, kwa madhumuni ya urahisishaji wa utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati kwa kutekeleza kazi maalum pale itakapoona inafaa.

(2) Muundo, taratibu, masharti na mambo mengine yanayohusiana na kamati zilizoanzishwa utakuwa kama itakavyoelezwa na Bodi.

## SEHEMU YA NNE
## MKURUGENZI MKUU NA WATUMISHI WENGINE WA TAASISI

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

**25.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sayansi ya afya au fani nyengine yoyote inayolingana nayo kutoka katika taasisi inayotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka saba katika fani ya sayansi ya afya au fani inayolingana nayo; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu;

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**26.**-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu na atatekeleza kazi za kila siku za Taasisi.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu :

(a) ataongoza Taasisi katika mipango na utekelezaji wa sera na programu za Taasisi;

(b) ataendesha mambo ya Taasisi katika utoaji wa huduma bora na kwa ufanisi;

(c) atasimamia fedha, rasilimali na mali za Taasisi;

(d) ataandaa, atapendekeza na kutekeleza mpango mkakati, mpango kazi na mpango wa utekelezaji wa Taasisi;

(e) atahakikisha kwamba sera na kanuni za Taasisi zinatekelezwa na kwamba malengo yaliyokubaliwa, shabaha na viwango vya huduma vinafikiwa;

(f) atasimamia na kuinua utendaji mzuri wa Taasisi;

(g) atatekeleza majukumu yoyote mengine kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii kama atakavyopewa na Bodi;

(h) atahakikisha watumishi wote wanapatiwa mafunzo ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao na utendaji kwa kufuata maadili na uwajibikaji;

(i) atawajibika kwa mapato yote na matumizi ya Taasisi kwa mujibu wa Sheria husika;

(j) atasimamia mambo ya nidhamu ya wafanyakazi wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(k) atawasilisha kazi za Taasisi kwa Bodi; na

(l) atatekeleza jukumu lolote jengine kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Watumishi wa Taasisi

**27.**-(1) Bodi inaweza, kwa kufuata taratibu na masharti, kumuajiri mtumishi mwengine au kumuajiri mshauri elekezi au mtaalam ikiwa ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Taasisi.

(2) Uajiri wa watumishi unaofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utafanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma au Kanuni zake.

SEHEMU YA TANO
SAMPULI ZA KIBAOLOJIA KWA AJILI YA UTAFITI WA AFYA, NA UTAFITI KATIKA DAWA ZA KIASILI NA TIBA MBADALA

Madhumuni ya ukusanyaji wa sampuli za kibaolojia.

**28.** Bila kujali sheria nyengine yoyote, sampuli za kibaolojia kwa ajili ya utafiti wa afya zitakusanywa tu kwa madhumuni yaliyoainishwa katika mapendekezo ya utafiti.

Hifadhi ya sampuli za kibaolojia.

**29.**-(1) Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali, kuiteua Taasisi maalumu ya utafiti au kituo cha afya kuwa benki ya kibaolojia na kutoa au kufuta leseni katika namna itakavyoelezwa katika Kanuni.

(2) Taasisi ya utafiti au kituo cha afya kilichoteuliwa kuwa benki ya kibaolojia chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kinaweza:

(a) kupokea sampuli za kibaolojia kwa madhumuni ya kuzihifadhi;

(b) kuhifadhi mabaki ya sampuli ya kibaolojia kwa kipindi kisichozidi miaka kumi, isipokuwa Taasisi ikiidhinisha kipindi kirefu zaidi cha muda kwa sababu maalumu; na

(c) kuteketeza sampuli za kibaolojia ambazo uteketezaji wake utazingatia miongozo iliyoelezwa ya kuepuka athari za kibaolojia kwa mazingira chini ya usimamizi ya Taasisi.

(3) Benki ya kibaolojia itafuata masharti ya Sheria ya Afya ya Jamii na Afya ya Mazingira, Sheria ya Usalama na Afya Kazini na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

(4) Mtu ambaye anaweka sampuli za kibaolojia bila ya kuwa na leseni atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Thelathini za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi, au adhabu zote mbili.

Kusafirisha na kuingiza sampuli za kibaolojia.

**30.**-(1) Mtu hatosafirisha au kuingiza sampuli za kibaolojia bila kupata idhini ya maandishi ya Taasisi kama ilivyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

(2) Taasisi inaweza, kwa mapendekezo ya Bodi, kuruhusu kusafirisha au kuingiza sampuli za kibaolojia ikiwa vipengele vyote vilivyoelezwa katika makubaliano ya kusafirisha sampuli vimefikiwa.

(3) Mtu ambaye anakwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Thelathini au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi, au adhabu zote mbili.

Udhibiti wa sampuli za kibaolojia.

**31.**-(1) Mtu hatosafirisha sampuli yoyote ya kibaolojia isipokuwa apate idhini ya Taasisi.

(2) Mtu ambaye anasafirisha sampuli ya kibaolojia bila idhini ya Taasisi atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Thelathini au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi, au adhabu zote mbili, na sampuli zake za kibaolojia zilizosafirishwa zitataifishwa.

Utafiti katika tiba asili na mbadala.

**32.** Taasisi:

(a) itawezesha kufanyika kwa utafiti wa afya katika tiba asili au tiba mbadala ndani ya Zanzibar;

(b) itahakikisha kwamba taarifa za tiba asili na tiba mbadala zinasambazwa kwa wingi;

(c) itaimarisha mashirikiano ya utafiti baina na miongoni mwa watafiti wa tiba asilia na tiba mbadala; na

(d) itahakikisha kwamba hakuna katika utekelezaji wa Sheria hii kinachozuia wataalamu wa tiba asili ikiwa binafsi au kwa pamoja kulinda haki miliki zao na taaluma za asili zinazohusiana na mchakato wa utayarishaji wa dawa za tiba au dawa zenyewe.

## SEHEMU YA SITA
## HAKI MILIKI

Haki miliki.

**33.**-(1) Haki miliki yoyote inayotokana na, au inayohusiana na utafiti wa afya unaofanywa chini ya Sheria hii italindwa kwa mujibu wa Sheria ya Mali Bunifu Zanzibar.

(2) Taasisi itaiendeleza, itaitangaza na itaitekeleza sera ya haki miliki kwa madhumuni ya:

(a) kuainisha umiliki au haki ya kutumia haki miliki inayotokana na utafiti wa taasisi husika au kwa ushirikiano wa pamoja na taasisi nyengine za shughuli za utafiti na maendeleo;

(b) kuweka kanuni za Taasisi kuhusiana na namna gani ya kuainisha vyema, kutathmini, kulinda na kusimamia haki miliki kwa ajili ya maendeleo zaidi, kikawaida kupitia shughuli za kibiashara;

(c) kutoa mpango kazi uliowazi kwa ajili ya mashirikiano ya watafiti na watu wengine; na

(d) kutoa miongozo kuhusiana na maslahi ya kiuchumi yanayotokana na biashara za haki miliki.

(3) Baada ya Taasisi kuipitisha na kuitangaza Sera ya Haki Miliki, Waziri atatunga kanuni kwa madhumuni ya utekelezaji na kulinda haki chini ya Sera hiyo.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Taasisi.

**34.**-(1) Fedha na rasilimali za Taasisi zitatokana na:

(a) fedha zinazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku;

(b) fedha zinazopokelewa na Taasisi zinazotokana na bidhaa au huduma zinazotolewa na Taasisi;

(c) misaada halali, zawadi, michango, mikopo, urithi, au uwekezaji kama Taasisi itakavyopokea kutoka kwa mtu yeyote au taasisi; na

(d) fedha nyengine zozote itakazopewa au kupatikana kihalali na Taasisi kutokana na utekelezaji wa kazi zake au vyenginevyo.

(2) Taasisi itatekeleza kazi zake kwa mujibu wa misingi ya jumla ya fedha na itahakikisha kwamba, kadri iwezekanavyo, makusanyo yake yanatosheleza matumizi yake sahihi kwa mujibu wa mpango kazi mkakati.

(3) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Waziri anayehusika na fedha, kuamua kiwango cha mapato ambacho kitabakia kuwa mali ya Taasisi, na bakaa ya mapato hayo itachukuliwa na kupelekwa katika hesabu za Serikali.

(4) Miamala yote ya fedha ya Taasisi itafanywa na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine yoyote ya fedha.

Makadirio ya mapato na matumizi.

**35.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, katika kila mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya majadiliano na kutoa mapendekezo, makadirio ya mapato na matumizi ya Taasisi kwa mwaka unaofuata.

(2) Baada ya majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Taasisi itachukuliwa kuwa ni sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, makadirio ya mapato na matumizi yatajumuisha makadirio ya ziada.

(4) Makadirio ya mapato na matumizi ya Taasisi yataandaliwa kulingana na matakwa na masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na miongozo mengine yoyote inayoweza kutolewa na Serikali kila baada ya muda.

(5) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba malipo yote ya fedha za Taasisi yanafanywa kwa usahihi na kama yalivyoidhinishwa, na udhibiti sahihi unaendelezwa kwa mali zake na dhima zinazoingiwa na Taasisi.

Hesabu na ukaguzi.

**36.**-(1) Taasisi itawezesha kufanywa na kuwekwa vitabu sahihi na kamili vya hesabu vinavyoonesha mapato yote na matumizi ya Taasisi.

(2) Mkurugenzi Mkuu, kwa kuzingatia miongozo ya Taasisi, ataandaa kuhusiana na utendaji wa Taasisi, kwa kuzingatia kila mwaka wa fedha, taarifa za hesabu ambazo zitajumuisha:

(a) taarifa za fedha na taarifa ya mapato na matumizi; na

(b) taarifa nyengine zinazohusiana na mambo ya fedha za Taasisi kama zinavyohitajika chini ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(3) Ndani ya miezi mitatu ya ufungaji wa hesabu kwa kila mwaka wa fedha, hesabu zinazojumuisha taarifa za fedha za Taasisi kuhusiana na mwaka huo wa fedha zitawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti ya utekelezaji wa mwaka.

**37.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, ndani ya miezi miwili baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Waziri, ripoti ya mwaka inayohusiana na mwaka huo wa fedha ikijumuisha:

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Taasisi, pamoja na ripoti ya ukaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) ripoti ya Taasisi ya mwaka wa fedha huo; na

(c) taarifa nyengine kama Waziri atakavyohitaji.

(2) Waziri atawezesha nakala ya ripoti ya Taasisi kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi, ndani ya miezi miwili au mkutano mwingine wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kupokea ripoti hiyo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Kufungua hesabu ya benki.

**38.** Taasisi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, itafungua hesabu ya benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

**39.** Mtu ambaye:

(a) anadanganya, anaghushi, anabadilisha au anakusudia kudanganya, kughushi au kubadilisha leseni yoyote iliyotolewa na Taasisi;

(b) anatumia leseni kwa shughuli nyengine isiyokuwa shughuli iliyoidhinishwa na Taasisi;

(c) anazuia au anamkwaza afisa au mtumishi wa Taasisi kutekeleza majukumu yake aliyopewa chini ya Sheria hii;

(d) anakataa au anashindwa, bila ya sababu za msingi, kutoa taarifa kwa afisa au mtumishi wa Taasisi ambayo kisheria imetakiwa kutolewa chini ya Sheria hii;

(e) anafanya au anatoa taarifa au tamko la uongo au siyo sahihi wakati wa kuomba leseni au idhini yoyote ya maandishi; au

(f) anaenda kinyume na masharti yoyote ya Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii,

anakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Thelathini au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi, au adhabu zote mbili.

Adhabu ya jumla.

**40.** Mtu yeyote ambaye anakwenda kinyume na masharti ya Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii na hakuna adhabu iliyoainishwa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano, au adhabu zote mbili.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Uchunguzi wa majaribio ya dawa.

**41.**-(1) Mtu hatofanya uchunguzi wa majaribio ya dawa kwa wanadamu ndani ya Zanzibar bila ya kupata idhini ya maandishi ya Waziri.

(2) Namna, taratibu na mienendo mengine ya kupata idhini ya maandishi ya Waziri itaelezewa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(3) Mtu yeyote ambaye anakwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Kanuni.

**42.** Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**43.**-(1) Tangazo la Kisheria Nam. 125 la 2018 linafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kulikofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Tangazo la Kisheria lililofutwa litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 1 Aprili, 2020.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***